**Mikono mbali na nyasi yetu ya buffel! Wafugaji wa Kenya wanapinga ubinafsishaji wa bioanuwai zao**

Shirika la GRAIN pamoja na shirika la seed savers network Kenya



Wafugaji mara nyingi hupuuzwa kama wahifadhi wa bioanuwai barani Afrika.Licha ya matishio mbalimbali wanayopata, kama vile kufungwa kwa njia zao za uhamiaji, vita , ukosefu wa shule na huduma za afya, mifumo ya vyakula wanayosimamia inasalia kuwa aina ya kilimo inayostahimili Zaidi katika maeneo kavu wanayoishi isipokuwa ardhi na nyasi ambazo mifugo yao hulisha zibinafsishwe.

Hali mbaya Zaidi Kama hii inatishia jamii za wafugaji wa kimaasai na wakalejin katika jimbo la bonde la Ufa nchini Kenya. Jamii hizi mbili kwa sasa zimehusika katika vita vya kumzuia mtu binafsi kupata haki za ubinafsishaji kwa aina ya nyasi mbalimbali ambazo jamii zimetumia kwa mifugo yao kwa karne nyingi. Hali hii inaonyesha mfano wa jinsi

haki za uzalishaji wa mimea(PBRs aina ya hati miliki wa mimea) inaweza kudhoofisha wazalishaji wa chakula wa kiafrika na ni kwa nini bara nzima lazima lipinge vikali ubinafsishaji wa bioanuwai.

**Umuhimu wa nyasi ya buffel kwa wafugaji nchini Kenya**

Geofrey Letakaan mzee wa miaka 63 wa jamii ya kikalejin ambayo ni jamii ya asili ya wafugaji iishio kaunti ya Baringo, Kenya anukuu

"Nyasi za buffel zimekuwepo tangu zama za baba yangu, babu yangu mpaka zama za baba wa babu yangu," anasema Letakaan. "Nyasi hizi zina thamani kubwa.Walishwapo ng'ombe hunenepa katika kipindi cha miezi mitatu. Zipo nyasi kwaajili ya kuunda marobota ya nyasi zinazohifadhiwa kwaajili ya kulishia mifugo yakiwa katika umbo la mviringo ama mraba (hay for baling), na zinatumika pia kwaajili ya kuezeka paa la nyumba. Zamani, wazee walikuwa wakisema 'nangrongong', wakimaanisha 'zipo (nyasi za buffel) katika vilima' kama vile vilima vya Arabal na Mukutani……Watu wanapaswa kupanda nyasi hizi- wote."

Mtazamo wa Letakaan unaashiria mitazamo ya wengi katika kaunti ya Baringo, ambayo ni eneo la nyasi la Bonda La Ufa nchini Kenya. Katika kaunti hiyo pia wapo jamii ya Ilchamus ambayo ni sehemu ya jamii kubwa ya Maasai. Wakalenjin na wailchamus ni wafugaji wategemeao ng'ombe wao na mifugo mingine.

Wafugaji wa Baringo husifika kwa upandaji wa nyasi za African foxtail ambayo kwa kisayansi huitwa (*Cenchrus ciliaris*), kwa umashuhuri huitwa "nyasi za buffel". Tangu kale, wanajamii wamekuwa wakilisha mifugo yako nyasi hizi.jamii ya Ilchamus huziita nyasi hizi "Lhomer aingok" nayo jamii ya tugen, ambayo ni kabila ndogo ya wakalenjin, huziita "Lhomer Kwan". Jamii hizi huzitumia nyasi hizi kama lishe la mifugo kwa muda mrefu kwasababu zimeweza kustahimili aina mbalimbali za udongo, humea haraka hata kwa mvua kidogo na zimesifika kama nyasi zenye uwezo mkubwa wa kustahimili ukame.

Maeneo ya kaunti ya Baringo na sehemu zingine kame nchini Kenya, nyasi za buffel ni muhimu mno na zenye ufanisi katika matumizi yake. Licha ya kuzitumia kama lishe kwa mifugo, jamii pia hutengeneza marobota ya nyasi kwaajili ya kuuza na kuhifadhi kwaajili ya kulishia mifugo katika kipindi cha ukame. Zikiwa na kiwango kingi cha protini cha asilimia 12, nyasi hizi

hunenepesha haraka mifugo. Baadhi ya wanajamii wamekuwa wakijihusisha na biashara ya kununua mifugo iliyodhoofika kwa bei ndogo, kisha kuinenenpesha kwa virutubisho vya mlo wa nyasi za buffel, na kuiuza kwa bei ya juu baada ya miezi mitatu. Pia, mbegu za nyasi hizi huwa na bei ya juu sokoni, kuanzia Ksh 300(US$ 3) mpaka Ksh 750(US$ 7.5) kwa kilo moja.

Wanawake ndio huwajibika katika kulisha mifugo katika jamii za wafugaji nao wanaume huenda malishoni. Hivyo wanawake, hutegemea kwa kiasi kikubwa kuunda malobota ya nyasi na kuhifadhi nyasi za buffel, hususani katika kulisha mifugo midogo (ndama) nyakati za kiangazi, wakati lishe ni nadra.

“Ninakwenda tu katika ghala, na kuchukua lobota na kuwalisha ndama na mbuzi,” anasema Shalline Parkolwa, wa miaka 29. Anatambua kuwa ndama wakilishwa vyema, hawatohitaji kunyonya sana. Hivyo maziwa mengi yatapatikana kwaajili ya familia, hivyo kuathiri vyema lishe na uhuru wa chakula, hususani kwa watoto na wazee. Zaidi ya hayo wanaume wanapojenga nyumba, wanawake hupewa jukumu la kusaka nyasi za kuezeka. Nyasi za buffel ni nzuri mno kwa kuezekea kwasababu mirija yake ni mirefu na imara. Wanawake pia wanaweza kupata mapato kwaajili yao binafsi na kujikimu kwa mahitaji ya nyumba zao kwa kuuza mbegu za nyasi ya buffel.

**Kuwasili kwa Murray Roberts**

Kwa miongo michache iliyopita, mtu aitwaye Murray Roberts, akifahamika kwa wenyeji kama “Omari” amekuwa akiongoza jitihada  za kujaribu kubadili uratibu wa asili(wa wenyeji) wa nyasi za buffel – kutoka katika mfumo wa umilikaji wa pamoja wa ardhi na ufugaji kuwa katika mfumo wa kibinafsi wa umilikaji wa ardhi na kilimo cha kina




***Robert Murray, mkurugenzi wa RAE, mmoja wa wafanyikazi wake katika duka lake la nyasi Baringo Februari 17, mwaka wa 2021. Picha: Seed Savers Network (SSN)***

1. Wakalejin ni kundi la jamii ambalo linatoka kaunti ya Baringo katika jimbo la bonde la ufa nchini Kenya.
2. AFSA 2018 .Ufugaji: uhuru wa chakula katika kitendo. Inapatikana kwa https://afsafrica.org/case-studies-pastoralism/
3. Wanajamii wa eneo hilo kwa kushindwa kutamka kwa kushindwa kutamka jina lake kwa usahihi humtaja kama 'Omari'

Roberts ni raia wa Kenya ambaye anatokana na walowezi wa kizungu waliopata ardhi eneo la Baringo nyakati za utwaaji ardhi kwa hila wa ukoloni wa maingereza, waliotengeneza biashara kubwa kubwa za familia zao kwenye mashamba, maeneo ya hifadhi  na safari za utalii. Mwaka 1982, Roberts aliasisi kampuni ya uhifadhi iitwayo, Rehabilitation of Arid Enviroment (RAE) Trust, ili "kubadili maeneo kavu yenye mmomonyoko kuwa tambarare zenye faida kwa maslahi ya watu na mazingira". Kampuni ya RAE imekuwa ikijaribu kufanya hayo kwa kudahili wanajamii kwenye mipango ya uzalishaji wa nyasi za buffel nakushawishi wazee wenyeji kupeana ardhi kwaajili ya kampuni na ukuzaji wa nyasi hii.

Robert Anukuu:

“Tulianza hapa mwaka 1982, kwanza kabisa Kwa sababu ya mfadhili, tuliruhusiwa kushughulikia jamii, hivyo tulikua na mashamba mengi wakati ule na wakati huu pia. Mfadhili alipobadilika, tuliweza kwenda Kwa watu binafsi. Hapo ndipo tuliweza kuona tofauti kumbwa Kwa kuwa tulipanda nyasi katika mashamba walimokuwa wamepanda mahidi, Bibi yangu ndiye aliyekuja na wazo hilo. Sasa wazo lote la kupanda nyasi kibinafsi limeshika kasi. Hili suala lote la nyasi limekuwa kiwanda hapa Baringo. Niwepo ama nisiwepo, kiwanda hiki (shughuli za uzalishaji nyasi) kitasonga mbele. Hakinitegemei Mimi Kwa sasa lakini najua Mashamba ya jamii nikitoka hapa, yataisha kwasababu hakuna yeyote katika jamii ambaye atayazingatia kwa sababu jamii hizi zinataka tu malisho ya mifugo. ”

Wenyeji wanasema jitihada za RAE zimebadili mahusiano baina yao na nyasi ya buffel. “Nyasi za buffel zimekuwepo hapa kwa miongo mingi.  Kitu pekee ambacho wanajamii hawakukifahamu ni uwezekano wa kibiashara yake.” asema mmoja wa jamii hii George Letakaan.

Leo hii wakaazi wengi wa jamii hizi, wanazalisha na kuuza mbegu za nyasi za buffel.Wengine wakiuza mbegu kupitia RAE, wakati wengine wakiuza kupitia Kerio Valley Development Authority (KVDA), kikanda cha serikali. Mwanajamii mmoja, Jackson Lekombe, ambaye KVDA na kwa ushirika kupitia Nooseya Self Help Group, ambao wanachama wake 25 wanajihusisha na biashara ya malobota ya nyasi na mbegu.

**Uporaji mbegu**

Juhudi za Roberts za kubinafsisha usimamizi wa mbegu za nyasi za buffel hazikukomea katika kujiepusha na jamii na badala yake kufanya kazi na watu binafsi wachache. Mwaka 2001, RAE ilianza mkataba wa uzalishaji mbegu za buffel. Mwaka 2012, kampuni iliagiza cheti cha Kinga ya Uelekeo (certificate of protective direction) – ambacho ni cheti cha uzalishaji mmea cha muda ikingonjewa cheti kamili cha ubinafsishaji.ombi la kutaka cheti kamili limewekwa pembeni kwa sababu katika orodha ya aina ya buffel grass,nyasi hii na ambayo Robert anadai ni mali yake

binafsi imeorodhoshwa na kuitwa Baringo 1 na wadhibiti wa mbegu nchini, Kenyan Health Inspectorate Services (KEPHIS).

Kwa kupewa cheti hiki, Baringo 1 iliongezwa katika orodha ya aina za mbegu za taifa la Kenya. Hii inamaana kwamba haiwezi kufanyiwa biashara bila idhini ya mmiliki. Mwaka 2014, Roberts alikwenda hatua nyingine na kufanya maombi ya haki ya uzalishaji mimea (PBRs) kwa Baringo 1, akilenga kutafuta umiliki-timilifu kwa gharama ya haki za wakulima. Roberts anakusdia kusajili aina nyingine tano za mbegu ya nyasi kwa kwenye haki za uzalishaji mimea (PBRs)

4 vipengele vya historia hii ya familia vimeelezwa kwenye tovuti ya kampuni inayoendeshwa na uhusiano wa Murray Robert

5 http://robertssafaris.com/our/history

6[1] Tazama sehemu ya uharibifu wa ardhi na ukidhi katika ," *Land Degradation and Desertification: Assessment, Mitigation and Remediation*," edited iliyoharirirwa na Pandi Zdruli, Marcello Pagliai, Selim Kapur, Angel Faz Cano, Springer Science & Business Media, 2010, p.117.

7 mahojiano iliyofanywa na shirika la mbegu la seedsavers, machi 2020

8 kifungu cha 18 cha sharia ya mbegu ya [Kenyan seed and plant varieties act] mwaka wa 2012 iliweka masharti ya kutoa haki/hati miliki za wafugaji wa mimea.Kifungu cha [2] kinasema kwamba mwombaji haki za umiliki wa mimea lazima awe ni mtu aliyezalisha au kugundua aina ya mmea husika au mrithi katika hatimiliki, na marshart ya sehemu ya kwanza ya jedwali la nne yatakuwa na athari kuhusu vipaumbele kati ya watu wawili au Zaidi ambao kibinafsi wamezalisha au kugundua aina ya mmea.

Chini ya Sheria ya Mbegu na Aina za Mimea ya mwaka 2012 ya nchi ya Kenya – ambayo inatokana na toleo la Mkataba Umoja wa Ulinzi wa Aina Mpya za Mimea (Union for Protection of New Plant Varieties Convention, UPOV 1991) mwaka 1991 – mzalishaji yeyote awe wa umma ama binafsi, mwenyeji ama mgeni anaweza kufanya ombi na kupata haki-hodhi juu ya aina mpya ya mmea waliyoigundua ama kuzalisha. Mkataba huu unaweza kuhusisha, aina ya mimea inayotumiwa na wakulima. Na hapo ndipo mgogoro kuhusu nyasi za buffel za RAE unapoibuka.

Roberts anajaribu kuleta madai ya umiliki wa bayoanuai ya jamii ya wafugaji. Eresia Erige, mwanajamii wa Baringo anasema kwamba kadiri jamii walivyozidi kupata uelewa kuhusu maombi ya Roberts ya haki ya uzalishaji wa mbegu yao, wazee kutoka jamii hizi walikwenda milimani na kukusanya sampuli kwaajili ya kufanya ulinganifu na aina zinazozalishwa na RAE. Waligundua zilikuwa ni nyasi za aina moja. Kwa Erige, “nyasi zile ni za milima na hivyo, mbegu zake na kilimo chake kwa ujumla kinapaswa kuwa cha wote na si kubinafsishwa.”

Wanafarijiwa na katiba ya Kenya, iliiopitishwa upya mwaka 2010 inayoratibu kwamba jamii za wenyeji zitakuwa na haki ya "umiliki wa aina ya mbegu na mimea ya asili/jadi, sifa zake tofauti na matumizi yake". Kwa msingi wa kikatiba, jamii za Baringo zinapaswa kuwa na haki ya kijamii juu ya nyasi za Buffel. Hata hivyo, Sheria ya Mbegu na Aina za Mimea ya mwaka 2012 ina mkanganyiko wa kikatiba ambapo inaruhusu watu kama Roberts kutwaa haki binafsi juu ya nyasi za buffel. Matokeo yake, kuna mgogoro baina ya haki za wazalishaji na haki za wakulima katika Kenya.

Kerio Valley Development Authority (KVDA) pia wamepinga ombi ya Roberts ya kutaka apatiwe Haki ya uzalishaji Mimea, ( PBRs). Katika barua kwake (Roberts) ya mwaka 2016, KVDA ilisema kuwa imekuwa ikijaribu na kuzalisha *Cenchrus ciliaris* tangu mwaka 2001 na tayari ilishaziingiza nyasi kwenye mchakato wa kitaifa wa majaribio. Ilitoa hoja kuwa RAE Trust isingeweza kuzalisha aina ilizoziwasilisha kwa kuwa haikuwa hata na programu ya uzalishaji wa mmea.

Zaidi, KVDA ilisisitiza kuwa nyasi za buffel zinapaswa kumilikiwa na umma na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo ya Kenya (KALRO) ndiyo ipewe jukumu la usimamizi kwa niaba ya maslahi ya umma.

KALRO wanabainisha kuwa *Cenchrus ciliaris* ni (apomictic). Hii ina maana kuwa inajizalisha kupitia jinsi moja kwa kupitia mbegu. Yeyote anayedai kuwa ameunda aina mpya ya mbegu za nyasi hizi atapaswa afafanue hatua za uzalishaji alizozipitia. Hadi leo, RAE wameshindwa kutoa taarifa hiyo.Nyasi hizi zinamea na kukua katika kaunti nyingine humu nchini ikiwemo Kilifi, Marsabit, Mandera, Kitui na Makueni. Kwa maoni ya shirika la KALRO, kati ya *Cenchrus ciliaris* lazima kunapatikana *Baringo* miongoni mwa nyasi tofautitofauti za aina ile kwa asilima 99.



***Wafugaji wa nooseiya /wakulima kutoka jamii ya ilchamus, mwezi wa wa februari 11 mwaka wa 2021.Picha: Seed Savers Network (SSN)***

Mwaka 2016, KEPHIS iliandaa kikao na Roberts, jamii zamitaa, KVDA na KALRO ili kutafuta suluhisho juu ya mgogoro. Katika kikao hicho, mashirika ya umma ikiwamo Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, zilikataa ombi la Murray ya kupatiwa PBR zikitamka kuwa aina ya nyasi alizokuwa akiziombea ubinafsishaji, zilikuwa ni za "umma" na zilikuwa zinamea bila upanzi na kwa hivyo kuwa za kiasili. Lakini Murray hakukubali. Alikuwa akiharibu kikao kwa kusimama na kutuhumu jamii kwa kupora "mbegu yake". Murray alidai kuwa ni yeye pekee ndiye alikuwa na "haki ya uzalishaji wa nyasi ya buffel, na jamii, KVDA na wazalishaji wengine wa mbegu walikuwa wakikiuka sheria.

9 sheria ya Kenya.katiba ya Kenya.kifungu cha 11.3(b) inapatikana katika http://kenyalaw.org/kl/index.php?id=398

10kulingana na hati ambazo zimepitishwa na waandishi

11 kulingana na shirika la KARLO

12 mahojiano yaliyofanywa na shirika la seed savers network Kenya mwezi wa tatu mwaka wa 2020

**Kipi ki mashakani?**

Kilicho mashakani katika mgogoro huu ni haki za wakulima kuhifadhi, kubadilishana na kuuza mbegu za nyasi za buffel. Ikiwa PBR itatolewa, hawataweza kuzalisha ama kuzifanyia biashara mbegu bila ruhusa ya Roberts na malipo ya mrahaba kwake. Hili litaathiri moja kwa moja maisha ya wanajamii wenyeji ambao daima wamezitumia na kuzitegemea. Kwa hili la Baringo 1, jamii za wenyeji na maofisa wa umma hawaamini kama Roberts alifanya kazi ya uzalishaji kama anavyodai. Wanapinga kwa urasmi uhalali mawasilisho yake katika mamlaka za usajili na haki za wazalishaji mimea.

Ni muhimu kukumbuka kuwa RAE haiko peke yake katika kutafuta umiliki wa nyasi za buffel. KALRO na KVDA pia ni taasisi ambazo zinanuia kupata uhodhi na biashara ya nyasi za buffel. Ugomvi baina yao unachochewa na ukweli kuwa RAE iliwapiku ujanja wengine hao wawili katika mchakato wa usajili wa aina hiyo yam mea. “KARLO pia inayo inatafuta njinsi itakavyo pita wengine kwa usajili. Tatizo si taasisi yeyote, lakini sheria ya mbegu itokanayo na UPOV 1991, ambapo jamii inaendelea kutaabika, bayoanuai inaendelea kuharibiwa, na haki za wakulima hazilindwi,” anasema Daniel Wanjama, Mkurugenzi wa seed savers network nchini Kenya.

Hivyo hali ya mvutano ingali ipo kwa jamii za Baringo. Ombi la PBR ya Murray hadi sasa halijakamilishwa na KVDA imechukua hatua za kisheria kuzuia jaribio hilo. Kwa sasa Murray Roberts na RAE Trust inaendelea kuongeza na kuuza mbegu hii. Hata hivyo, kwasababu ya jambo hili kushika hisia za wengi, hatishii tena jamii za wenyeji kuhusu “kupanda mbegu zake”.

Kwa sasa, wanajamii wa Baringo wanamekusudia kuendelea kupanda nyasi za buffel na kupuuza madai ya Murray juu ya mbegu zao. Katika safari hii, wanaungwa mkono na Wizara ya Kilimo, ambayo imejitokeza na kusema haki ya uzalishaji juu ya Baringo 1 isipeanwe.

Hata hivyo, hii “ni jitihada isiyo na faida kuona kwamba haki za wakulima zilikuwa tayari zimegandamizwa wakati aina ya Baringo 1 iliposajiliwa katika orodha ya Taifa ya Aina za Mimea,” anasema Domonic Kimani kutoka shirika la seed savers network Kenya.

**Kama Jamii tunakataa ubinafsishaji wa mbegu zetu na RAE, KVDA, ama umiliki wowote wa kibinafsi.**

Mgogoro huu unaonesha namna sheria na kanuni zinazodhibiti sekta ya mbegu zimeundwa kuyanufaisha makampuni ama watu binafsi na kupuuza haki za wakulima na jamii za mtaa.

Vuta nivute hii ya nyasi ya buffel, Murray anatumia tu mlango tu wa ubinafsishaji mbegu uliotengenezwa na Sheria ya Mbegu na Aina za Mimea ya Mwaka 2012 ya nchi ya Kenya – itokanayo na UPOV 1991.



***Shalline Parkorwa, mfugaji/mkulima kutoka jamii ya ilchamua akionyesha nyasi ya buffelmwezi wa February 11, mwaka wa 2021 kijiji cha salabani Baringo. Picha: Seed Savers Network (SSN)***

Ilikuwa ni suala la muda tu kabla RAE hawajakimbilia katika mkondo wa sheria kudai udhibiti wa aina ya mmea ambao maarifa kuuhusu ni ya watu wote wa jamii. Ulinzi wa kweli utarejea ambapo itakapoitupilia ambali sheria ambazo msingi wake ni UPOV. Jaribio la hivi punde la

KVDA na mamlaka nyingine za umma kumzuia Murray asipate PBR lazima zionekane kwa namna zilivyo: mvutano wa ubinafsishaji mbegu. Hata kama jaribio la RAE kupata PBR lisipofaulu, wafugaji na wakulima wa Baringo watapoteza haki zao kutumia, kuhifadhi na kuzalisha nyasi za Baringo 1, kutoka kwa KVDA ama yeyote mwingine. Jaribio lolote la kulinda mmea huu wa millennia tena wenye utajiri wa utofauti lazima lifanyike kupitia wadau wake ambao ni wafugaji, wakulima na jamiii ambazo zimeitunza mimea hii kwa vizazi vingi.

13 Mahojiano na shirika la seed savers

14 Kulingana na hati zilizoonekana na waandishi

**Jedwali 1: Mpangilio wa matukio**

| Kipindi/Mwaka | Tukio |
|---|---|
| **Hadi mwaka 1982** | Wafugaji wakalenjin na wamaasai walikuwa wakichunga na kulisha mifugo yao nyasi za buffel katika nyanda zao. |
| **1982** | Murray Roberts kupitia  shirika lisilo la kiserikalila  Rehabilitation of Arid Enviroment (RAE) Trust, anaanzisha program ya nyasi za buffel inayowashirikisha wanajamii wenyeji wa Baringo |
| **1991** | Mkataba wa UPOV unafanyiwa marekebisho huko Geneva na kuwekwa katika hali yake ya sasa |
| **1999** | Kenya inakuwa mwananchama wa UPOV |
| **2001** | Murray Roberts anaanza kuzalisha mbegu za nyasi za buffel |
| **2010** | Kenya inapata katiba mpya ambayo inatambua haki za jamii za mtaa juu ya mbegu zao na maarifa yao mbalimbali ya jadi. |
| **2012** | RAE Trust inapewa  cheti ya mwelekeo wa kinga kwenye aina ya nyasi ya Buffel, shahada ilotolewa na  KEPHIS |

| | |
|---|---|
| **2012 (Desemba)** | Mabadiliko ya Sheria ya Mbegu na Aina za Mimea ya mwaka 2012 ya Kenya yanapitishwa |
| **2014** | Mzozo baina ya jamii za Baringo, RAE Trust na KVDA juu ya ombi ya kupata Haki za Wazalishaji Mimea yaliyofanywa na RAE |
| **2016** | Kenya yajiunga rasmi na UPOV 1991 na kuanza kuwajibika kiutimilifu kutekeleza masharti ya mkataba |
| **2017** | Serikali inatangaza kuchapisha cheti cha misho kuikabidhi RAE haki ya kuuza nyasi za Buffel aina ya Baringo 1 |